

USHAIRI MASWALI NA MAJIBU MODELI 2362021544

 atikaschool.org/ushairi-maswali-na-majibu/ushairi-maswali-na-majibu-modeli-2362021544

USHAIRI

Eti

Mimi niondoke hapa

Niondoke hapa kwangu

Nimesaki, licha ya risasi

Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi

Siondoki

Siondoki siondoki

Niondoke hapa kwangu!

Kwa mateke hata na mikuki

Marungu na bunduki, siondoki

Hapa

Siondoki

Mimi ni Pahame!

Niondoke hapa kwangu!

Fujo na ghasia zikizuka

Na kani ya waporaji, siondoki

Haki

Siondoki

Kwangu siondoki

Niondoke hapa kwangu!

Nawaje; waje wanaokuja

Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe

Siondoki

Ng'oo hapa kwangu!

Katizame chini mti ule!

Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi

Nende wapi?

Si hapa kitovu changu

Niondoke hapa kwangu

Wangawa na vijikaratasi

Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu
Siondoki
Sihitaji karatasi
Niondoke hapa kwangu
Yangu mimi ni ardhi hii
Wala si makaratasi, siondoki

Maswali

- a) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini (alama 2)
- b) Taja masaibu anayopitia mzungumzaji (alama 4)
- c) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)
- d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)
- e) Tambua matumizi ya mbinu ya usambamba (alama 2)
- f) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)
- g) Tambua idhini moja ya mtunzi (alama 1)
- h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (alama 3)
 - (i) Karatasi
 - (ii) Nimesaki
 - (iii) kitovu

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA - USHAIRI

- 1.
 - a.
Ni shairi huru kwa sababu mshairi ametumia (i) mishata mf. katu, eti, niondoke
Shairi lina umbo la paa la nyumba
Matumizi ya alama za uakifishaji kwa wingi (al. 2)
 - b.
 - (i) Anatishwa kwa risasi
 - (ii) Kupigwa mateke na mikuki
 - (iii) Kuponda mali yake
 - (iv) Kuletewa hatimiliki bandia (mwalimu akubali hoja nyingine yoyote) Al. 4
 - c.
 - (i) Huzuni
 - (ii) Ujasiri (2 x 1)
 - (iii) Uchungu
 - d.
Shairi lina beti saba
Kila ubeti una mishororo sita
Lina umbo la paa la nyumba (3 x 1)
 - e.
Usambamba – Ni urudiaji wa kiwango cha sentensi, kirai (n.k)
mf.
 - (i) Niondoke, mimi niondoke hapa, niondoke hapa kwangu
 - (ii) Siondoki, siondoki, siondoki niondoke hapa kwangu (2 x 1)

- f.
Mshairi anasema kamwe hatoki kwake. Anaashiria chini ya mti waliozikwa babu zake na kusisitiza kwamba hawezi akaondoka (al. 3)
- g.
Inkisari –
(i) Sendi – Siendi Nende wapi – Niende wapi
(ii) Kuboroga sarufi mf yangu mimi ni ardhi hii – Ardhi hii ni yangu mimi (1 x 1)
- h.
Karatasi – Hati miliki
Nimesaki – Nimebaki
Kitovu – Asili

(al. 3 x 1)